BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Febuari, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya mwaka 2016/2017.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

107. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa kuwa Posho la Madiwani halijaongezwa tokea utawala wa Awamu ya 5 na kwamba Madiwani wanastahiki kuongezewa maposho kulingana na kuongezeka kwa makusanyo.

a) Je, makusanyo ya Manispaa yameongezeka kwa asilimia ngapi kwa mwaka 2015/2016.

b) Je, ni asilimia ngapi ya maposho ya Madiwani yaliongezeka.

108. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwa kuwa katika vikosi vya SMZ, baadhi ya watumishi wake walikuwa ni watumishi wa JWTZ na kwa sababu muda wa utumishi wao ulikoma toka jeshini na wakapewa mkataba kwenye vikosi vya SMZ na kuongezewa muda kwa zaidi ya mara mbili, wakati sheria ya utumishi imeeleza wazi kuhusu sifa za mtumishi ambae anastahiki kuongezewa muda baada ya vipindi viwili.

a) Je, sababu gani za msingi zilizopelekea kuongezewa muda zaidi ya mara mbili kwa maofisa hao.

b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwaongezea muda watumishi waliokwishastaafu ni kuwanyima fursa vijana ambao tumewasomesha na wana uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu.

c) Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni kukiuka sheria yetu ya Utumishi wa Umma tuliyoitunga sisi wenyewe.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

75. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na kumbukumbu katika Jimbo la Chambani kama vile Mgagadu ambako ipo miembe ya makumbusho mjini Chambani na Jambangome.

Je, Mhe. Waziri unazijua kumbukumbu hizi na kama unazijua Wizara yako inachukua hatua gani katika kuhamasisha utunzaji wa kumbukumbu hizi.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

81. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Serikali ya Zanzibar inajitahidi kuzuia matendo ya udhalilishaji kijinsia hasa kwa watoto na wanawake lakini hata hivyo mambo hayo kwa sasa yamekithiri.

a) Je, Serikali imeweka mipango gani ya kuzuia au kumaliza kabisa udhalilishaji huo.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipiga marufuku kwa watoto chini ya miaka 18 kutembea nje ya nyumba zao baada ya saa 2 usiku, Je sheria hiyo bado ipo na kama haipo tena ilifanya hivyo kwa madhumuni gani.

c) Je, Serikali haioni kuwa kuwaachia watoto kutembea usiku ni kuongeza vitendo vya kubakwa.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

57. MHESHIMIWA SULEIMAN MAKAME ALI (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Kumejitokeza tatizo kubwa kwa wananchi wetu ambao ni wavuvi wa majongoo na makome kwa kuzuiwa kuvua mazao hayo wakati ambapo kazi hiyo inategemewa na watu wengi katika kuwapatia kipato na kupambana na maisha yao ya kila siku.

Je Serikali ina mpango gani wa kuwapatia kazi nyengine wananchi hao ambao wanategemea bahari na wanavua uvuvi huo.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

35. MHESHIMIWA DKT. MAKAME ALI USSI (Jimbo la Mtopepo) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kwa kuwa Miundombinu ni muhimu sana katika kukinga majanga mbali mbali yenye athari kubwa kwa maisha ya binaadamu. Na kwa kuwa ubunifu na uangalifu mkubwa huhitajika ili kuwa na miundombinu stahiki inayokidhi haja ya mahitaji ya kimaendeleo hasa kwa nchi kama yetu yenye ardhi ndogo inayoathiriwa sana na mmong'onyoko kupitia maji ya bahari na mvua ambayo husababisha mafuriko na hivyo kuleta hasara kwa Serikali na jamii.

(a) Je, Wizara yako ina utaratibu gani wa kupunguza au kuondosha tatizo hili la mmong'onyoko kwa kujenga miundombinu itakayosaidia kuihami ardhi hii.

(b) Je, kuna mpango gani utakaowezesha kutatua tatizo la mmon'gonyoko mkubwa unaoathiri makaazi ya wananchi kutokana na mafuriko na hata kuhatarisha miundombinu ya barabara ambayo inaelekea kupata athari za kubomolewa na maji yanayotiririka kwa kasi kuelekea daraja la Garagara katika Jimbo la Mtopepo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

37. MHESHIMIWA DKT. MWINYIHAJI MAKAME (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Barabara iendayo Benki ya CRDB Mkunazini ni "One-way". Hilo ni wazo zuri katika kupunguza msongamano wa gari.

Kwanini Barabara inayokwenda Benk ya CDDB ni mbovu na ina mashimo mengi tofauti na inayotoka Benki hiyo ya CRDB.

88. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kuendelea kutoa huduma za usafirishaji wa wananchi wake katika visiwa vya Unguja na Pemba, lakini sekta hii ya usafirishaji bado inaendelea na mfumo ule ule wa kusafirisha watu au wananchi kwa meli ambazo safari ya Unguja na Pemba huchukua siku nzima kutoka asubuhi mpaka jioni. Mpaka sasa sekta hii haijaonesha njia nyingine za haraka na za kisasa zaidi kusafirisha wananchi wake.

a) Je, Shirika la Meli bado linatumia mfumo wa kutoa huduma na halijiendeshi kibiashara.

b) Je, badala ya kutumia mfumo wa meli kubwa za kusafirisha wananchi, kuna mpango gani wa kununua boti kubwa za kisasa kwa ajili ya kuwapa unafuu wasafiri wake na kwenda na wakati wa kisasa na haraka zaidi.

c) Shirika hili linajikita zaidi kusafirisha wananchi wake kwa njia ya bahari, kwanini Serikali haiwekezi kwenye ndege hasa kwa kuzingatia kuwa wakati mwengine bahari huwa imechafuka vibaya sana.

<u>Wizara ya Afya</u>:

24. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Hospitali ya Chake Chake haina Chumba cha wagonjwa mahututi (ICU).

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga chumba hicho pamoja na kuweka vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili hiyo.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2016/2017.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya mwaka 2016/2017.

Zanzibar,
22 Febuari, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.